**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 01 Juni, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

130. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kabla ya ugatuzi, elimu ya msingi ilikuwa ikisimamiwa na Mkurugenzi wa Idara ya Msingi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Na kwa kuwa Serikali imefanya ugatuzi wa baadhi ya sekta miongoni mwao ni sekta ya elimu ya msingi.

(a) Je, baada ya ugatuzi kwa nini hakuna Idara ya Msingi inayosimamia elimu ya msingi.

(b) Je, katika ngazi ya Wizara chini ya Katibu Mkuu, kuna Afisa wa aina gani anayesimamia elimu ya msingi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

206. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inamiliki mali nyingi sana ikiwa ni pamoja na majengo, gari, mashamba huku Ofisi ya Rais, Fedha ndio msimamizi mkuu wa mali za Serikali kupitia Idara ya Uhakiki Mali. Kwa muda mrefu sasa Wizara ilitoa muongozo wa kuhifadhi mali zake kwa Mawizara na Taasisi za Serikali na mali hizi huhifadhiwa kwenye Daftari la Mali (Fixed Asset Register).

(a) Je, ni kiwango gani (rate) iliyotolewa kwa Mawizara na Mashirika ya Serikali katika utekelezaji kwa kufuata muongozo wa Wizara kwenye eneo la kushuka thamani (depreciation) hasa kwenye majengo, magari na meli.

(b) Je, ilipouzwa meli ya MV. Mapinduzi I utaratibu gani ulitumika katika uondoshaji wa mali ya Serikali katika kufanywa tathmini na kupigwa mnada kwa meli hiyo.

(c) Je, kuna utaratibu gani wa Wizara yako kupitia na kuhakiki mali za Serikali, na kama uhakiki umefanyika, mara ya mwisho ulifanyika mwaka gani.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

56. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kuna kampuni zilizosajiliwa Tanzania Bara, mfano “Insight Security”, Kihero na “Green West” zimeajiri wafanyakazi hapa Zanzibar.

(a) Je, haki na stahiki za wafanyakazi walioajiriwa na kampuni hizo zinasimamiwa na mamlaka ipi ya Serikali.

(b) Kwa nini baadhi ya makampuni haya hayana Ofisi hapa Zanzibar.

(c) Ni kwa nini makampuni hayo hayalipi kima cha chini cha mshahara kilichotangazwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

181. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika kipaumbele chake cha Bajeti 2020/2021 Serikali ilikusudia kusimamia ujenzi wa kituo cha kulelea wajasiriamali Pemba na kuimarisha uendeshaji wa kituo kama hicho kwa upande wa Unguja.

Je, ni hatua gani zilizofikiwa katika utekelezaji wa lengo hilo la kipaumbele.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

208. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa sehemu kubwa ya uchumi wa Zanzibar inategemea pia sekta ya uvuvi na katika kukuza matokeo mazuri ya uvuvi huo, Wizara yako inahitaji kutambua maeneo yenye kupatikana samaki kwa wingi (Fishing Ground) kama wanavyofanya wenzetu wanaotegemea uchumi wa bahari.

(a) Je, kwa hapa Zanzibar utaratibu wa kuyatambua maeneo yanayopatikana samaki kwa wingi (fishing ground) umeshaanza.

(b) Na kama bado haujaanza, Je, Serikali ina mkakati wa kuyatambua lini.

(c) Je, ni makundi mangapi ya vijana yaliyofaidika na elimu ya uvuvi wa aina hii, kwa visiwa vyote vya Unguja na Pemba.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

19. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwa kuwa Serikali imeahidi kuzifanya hospitali za “Cottage” kuwa za Wilaya, na kwa kuwa tayari zoezi hilo limeanza kwa Hospitali ya Micheweni.

Je, ni lini zoezi hilo litaanza kwa Hospitali ya Vitongoji "Cottage"

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

69. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kipindi kirefu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar inalidai Shirika la Ndege la Tanzania ATCL deni kubwa ambalo halijalipwa kwa madai ya kuhakiki madeni.

(a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya juhudi gani ya kuisaidia Mamlaka ya Viwanja wa Ndege Zanzibar (ZAA) kulipwa deni lao.

(b) Ni kiasi gani cha fedha ambacho Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar wanalidai Shirika la Ndege la Tanzania ATCL.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

97. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa skuli binafsi zipo kwa mujibu wa Sheria lakini pia zimeweza kuisaidia Serikali kupunguza idadi ya wanafunzi katika skuli za Serikali. Kuna malalamiko kwa baadhi ya skuli binafsi kwa wanafunzi ambao wanamaliza au wanatoka na kwenda kujiunga na skuli za Serikali kutowekwa katika skuli husika kwa mujibu wa sifa zao (combination).

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea wanafunzi hao kutopangiwa skuli kwa mujibu wa sifa zao.

(b) Je, Serikali haioni kuwa kufanya hivyo kunasababisha wanafunzi kufanya mitihani ya masomo ambayo hawayawezi na kusababisha ufaulu kuwa mdogo.

(c) Je, kuna tathmini yoyote imefanyika kujua uwezo wa wanafunzi na sifa zao kwenye masomo husika kama inachangia kufaulu au kutofaulu vizuri kwa mwanafunzi.

106. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli za Jimbo la Bumbwini zinaupungufu mkubwa wa walimu na kuna vijana wengi wanaojitolea.

Kwa nini tusiwaajiri vijana hawa ili kupunguza upungufu uliopo wa walimu.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**01 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**